

## JE, IKIWA NILIPATA CHANGO YA BCG?

Nchi nyingi nje ya Marekani hutumia chanjo ya BCG kama sehemu ya mpango wao wa kudhibiti ugonjwa wa Kifua Kikuu, hasa kwa watoto wachanga. Ufanisi wa chanjo ya BCG unatofautiana na ulinzi wa change hiyo dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu hupungua kadri muda unavyosonga. BCG inaweza kusababisha matokeo yasisyo ya kweli wakati wa uchunguzi wa ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa kutumia ngozi. Uchunguzi wa Ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa kutumia damu hauathiriwi na chanjo ya BCG na hautoi matokeo yasiyo ya kweli. Ikiwa umepokea BCG (kama chanjo au tiba ya kansa), uchunguzi wa Kifua Kikuu kwa kutumia damu unapendelewa.

CERTAMEN AD FINEM PERGIT

THE FIGHT CONTINUES TO THE END


**IDARA YA AFYA YA UMMA YA IOWA**
**MPANGO WA KUDHIBITI UGONJWA WA KIFUA KIKUU**

Jengo la Lucas State Office Building
321 East 12th Street
Des Moines, IA 50319-0075

**idph.iowa.gov/immtb/tb**


Machi 2018 Swahili

# Pata ukweli kuhusu Kifua Kikuu



**Idara ya Afya ya Umma ya Iowa**
**Mpango wa Kudhibiti Ugonjwa wa Kifua Kikuu**

**Kifua Kikuu (TB) sio tu ugonjwa wa zamani. Kote duniani, Ugonjwa wa Kifua Kikuu unaua watu zaidi kuliko magonjwa mengine yanayoambukiza, ikiwa ni pamoja na VVU. Ugonjwa wa Kifua Kikuu usiotibiwa unaua mmoja kati ya waathirika wake wawili.**

## JE, UGONJWA WA KIFUA KIKUU NI UPI?

Kifua Kikuu ni ugonjwa unaosababishwa na bakteria (vimelea) ambayo huenea kutoka kwa mtu hadi kwa mtu mwingine kupitia hewa. Mara nyingi, Kifua kikuu huathiri mapafu (Ugonjwa wa Kifua Kikuu wa mapafu) lakini pia Kifua Kikuu inaweza kuathiri sehemu zingine za mwili, kama vile ubongo, nodi za limfu au mgongo.

## JE, KIFUA KIKUU INASAMBAZWA KWA NJIA IPI?

Vidudu vya Kifua kikuu huenea wakati mtu mwenye ugonjwa wa Kifua Kikuu anakohoa, anapiga chafya, anaongea au anaimba. Watu ambao wanapumua hewa iliyo na vimelea vya Kifua Kikuu wanaweza kuambukizwa. Si kila mtu aliyeambukizwa na bakteria ya Kifua Kikuu anagua. Matokeo ya maambukizi ni hali mbili zinazohusiana na Kifua Kikuu: maambukizi ya Kifua Kikuu yasiyojitokeza mwilini (Latent TB -LTBI) na ugonjwa wa Kifua Kikuu.


## JE, KUNA TOFAUTI GANI KATI YA MAAMBUKIZI YA KIFUA KIKUU YASIYOJITOKEZA MWILINI (LTBI) NA UGONJWA WA KIFUA KIKUU?

### LTBI

Watu walio na LTBI wana vimelea vya ugonjwa wa Kifua Kikuu katika miili yao lakini hawagonjeki kwa sababu vimelea hivyo havijitokezi. Watu wenye LTBI ambayo haitibiwi wamo katika hatari ya kuambukizwa ugonjwa wa Kifua Kikuu. Matibabu ya LTBI yanapendekezwa sana ili vijidudu vya Kifua kikuu visijitokeze mwili na kusababisha Ugonjwa wa Kifua Kikuu.

### Ugonjwa wa Kifua Kikuu

Watu wanaougua ugonjwa wa Kifua Kikuu wanagonjeka kutokana na vimelea vya Kifua Kikuu mwilini wao. Dalili za ugonjwa wa Kifua Kikuu unaoathiri mapafu ni: kikohozi kwa zaidi ya wiki tatu, kupoteza uzito kusikoelezwa, kupandwa na joto mwilini, kutokwa na jasho usiku na uchovu. Watu wanaougua ugonjwa wa Kifua Kikuu wanaweza kueneza vimelea vya Kifua Kikuu kwa watu wengine. Ugonjwa wa Kifua Kikuu unaweza kuponywa kwa kutumia matibabu yenye ufanisi. Ugonjwa huu ukiwachwa bila kutibiwa, watu wanaogua Kifua Kikuu wanaweza kuwa wagonjwa sana na kuaga duniani.



## JE, UNAFANYAJE UCHUNGUZI WA UGONJWA WA KIFUA KIKUU?

### Uchunguzi wa ngozi

Uchunguzi wa ngozi ndio uchunguzi unaotumika zaidi kuchunguza ugonjwa wa Kifua Kikuu. Uchunguzi huu unafanywaa kwa kudunga sindano ndogo ya maji (tubakulini) chini ya ngozi ya mkono wako. Mtoa huduma wako wa afya ataangalia mkono wako kwa saa 48-72 baada ya uchunguzi wa ngozi wa kuchunguza ugonjwa wa Kifua Kikuu ili kujua kama matokeo ya uchunguzi yanaonyesha "kuwepo kwa Kifua Kikuu" au "hakuna Kifua Kikuu."

### Uchunguzi wa Damu

Njia nyingine ya kupima ugonjwa Kifua Kikuu ni Uchunguzi maalum wa damu. Uchunguzi wa damu unaonyesha jinsi mfumo wako wa kinga unavyoathirika na vimelea vinavyosababisha Kifua Kikuu. Mtoa huduma wako wa afya atavuta damu kutoka kwa mkono wako ili kufanya uchunguzi huu. Ziara moja tu inahitajika, na matokeo hutokea katika siku chache.

| LTBI | UGONJWA WA KIFUA KIKUU (mapafuni) |
|---|---|
| Uchunguzi wa Ugonjwa wa Kifua Kikuu Unaonyesha kuwepo kwa Kifua Kikuu (uchunguzi wa ngozi au damu) | Uchunguzi wa Kifua Kikuu (ngozi au damu) mara nyingi huonyesha kuwepo kwa ugonjwa wa Kifuaa Kikuu mwilini lakini unaweza kuonyesha kutokuwepo kwa ugonjwa wa Kifua Kikuu kukosa kubainisha ugonjwa |
| Eksirei ya kawaida ya Kifua | Eksirei Isiyo ya Kawaida ya kifua |
| Hakuna dalili | Dalili: kukohoa kwa zaidi ya wiki 3, kupoteza uzito kusikoelezeka, kupandwa na joto, kutokwa na jasho mwilini usiku uchovu |
| Sio Ugonjwa wa kuambukiza | Inaweza kuambukiza |
| Matibabu ya LTBI yanapendekezwa | Huponywa kwa kutumia antibaiotiki |



## JE, IKIWA UCHUNGUZI WA KIFUA KIKUU UNAONYESHA NINA KIFUA KIKUU?

Kama aidha uchunguzi wa ngozi au damu unaonyesha kuwa una ugonjwa wa Kifua Kikuu, basi huenda umeambukizwa vimelea vinavyosababishwa Kifua Kikuu. Mtoa huduma wako wa afya ataamuru ufanyiwe Eksirei (X-ray) ya kifua ili kuhakikisha kwamba maambukizi ya Kifua Kikuu hayajaendelea na kuwa ugonjwa wa Kifua Kikuu. Ikiwa unakohoa au Eksirei ya Kifua sio ya kawaida, uchunguzi wa ziada unaweza kuwa muhimu.

## IKIWA UCHUNGUZI WANGU WA KIFUA KIKUU UNAONESYSHA NINA KIFUA KIKUU, NINAWEZA KUMEZA DAWA?

Ndiyo, matibabu mara nyingi hupendekezwa kwa watu ambao uchunguzi wao wa ugonjwa wa Kifua Kikuu unaonyesha wanaugua Kifua Kikuu. Matibabu ya LTBI kwa kawaida huwa ni dawa za antibaiotiki kwa miezi 6-9. Kwa kumeza dawa za antibaiotiki ili kutibu LTBI, unaweza kupunguza hatari yako kuugua na ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa asilimia 70-90 katika maisha yako. Ni muhimu kumeza dawa za antibaiotiki zote ili kuzuia maendeleo ya LTBI na ugonjwa wa Kifua Kikuu.

Ugonjwa wa Kifua Kikuu unaweza kutibiwa kwa kumeza antibaiotiki kadhaa kwa miezi 6-12. Ni muhimu sana kwamba watu wanaougua ugonjwa wa Kifua Kikuu kumaliza dawa zao na kuzinywa kama ilivyoagizwa. Ikiwa watu watawacha kumeza dawa za antibaiotiki bila kumaliza muda unaohitajika, huenda wakagonjeka tena. Ikiwa hawamezi dawa za antibaiotiki kwa usahihi kama ilivyoagizwa, vimelea ambavyo bado vinapatikana vinaweza kuunda kinga dhidi ya dawa za antibaiotiki.

Idara ya Afya ya Umma ya Iowa, Mpango wa Kudhibiti Ugonjwa wa Kifua Kikuu hutoa dawa za kutibu LTBI na ugonjwa wa Kifua Kikuu bila malipo.